



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA UYUI

**TANGAZOKWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA  
WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU**

(Limetolewa kwa kuzingatia Kanuni ya 7 (1)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu, ambapo jumla ya **Shilingi 332,296,570** zimetengwa katika robo ya pili (II) ya Mwaka wa fedha **2024/2025**. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za Serikali za Mtaa zilizopo katika maeneo yetu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- i. Kikundi cha Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha Utambuzi na Halmashauri.
- ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za Ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za Ujasiriamali.
- iii. Kikundi cha Wanawake na Vijana kiwe na idadi ya wanakikundi watano (5) na kikundi cha Watu wenyewe Ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) Mtu mwenye Ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenyewe ulemavu endapo Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa zingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.
- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- v. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenyewe akili timamu na wenyewe umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenyewe umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kuitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasilana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Kwa vikundi ambavyo walituma maombi na hawakupata mkopo wanatakiwa kurekebisha maandiko yao na kuomba mkopo upya, Kikundi kitafanya shughuli ya kusajili kikundi na kutuma maombi ya mkopo.

#### A: USAJILI WA KIKUNDI

Kikundi kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo:-

- i. Barua ya kikundi kuomba Usajili iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji.
- ii. Muhtasari wa kikundi kuomba usajili
- iii. Katiba ya kikundi iliyosainiwa na wanachama wote.
- iv. Namba za NIDA kwa kila mwanachama
- v. Namba za simu kwa kila mwanachama

#### B: MAOMBI YA MKOPO

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo:-

- i. Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji.
- ii. Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo
- iii. Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyon dani ya mfumo.
- iv. Taarifa ya akaunti ya benki iliyohai (Bank statement).

Usajili wa maombi utaanza siku ya Jumatatu tarehe **17/03/2025** na mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **18/04/2025** siku ya Ijumaa.

Tangazo hili limetolewa na: -



DR. Kija A. Maige  
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Wilaya  
Halmashauri ya Wilaya  
UYUI

